

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Tel.025-2957388

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P. 73,

TUNDUMA – SONGWE
FAX NO. 025-2957395

18.09.2022

Email: td@tundumatc.go.tz

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI- LIMERUDIWA

Mkurugenzi wa Mji wa Tunduma anawatangazia watazania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Mji Tunduma kuomba nafasi za kazi zifuatazo:

KATIBU MUHTASI III- NAFASI NNE (4)

Sifa za mwombaji

1. Awe na elimu ya kidato cha nne, waliohuzulia mafunzo ya uhazili na kufaulu hatua ya tatu (**NTA Level 5**). Wawe wamefaulu somo la hati mkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chou chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti cha program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

Kazi za Kufanya

1. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
2. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
3. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake wa kazi, majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za ofisi.
4. Kusaidia kupokea majalada, kusaidia kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu walipo na kukusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu husika.
5. Kusaidia kutunza taarifa, kumbukumbu za matukio

Ngazi ya Mshahara TGS B

Masharti ya Jumla kwa waombaji wote

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na asizidi miaka 45
2. Barua ya maombi imbatane na vitu vifuatavyo
 - i. Wasifu wa binafsi wa mwombaji wa hivi karibuni (Curriculum Vitae) wenye anuani, namba za simu na wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika
 - ii. Nakala ya Cheti cha kuzaliwa, cheti cha Kidato cha nne na Vyeti vya Taaluma (**NTA Level 5**)

- vi. Matokeo ya muda (provisional / testimonials / statement of results) hayatapokelewa
 - vii. Barua ya maombi iandikwe kwa lugha ya Kiswahili /kiingereza
 - viii. **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 27/09/2022 saa 9:30 alasiri**
3. Wale watakaochaguliwa kwaajili ya usaili ndio watakaoitwa
 4. Halmashauri haitahusika na Gharama za kuja kwenye usaili
 5. Maombi yote yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa

Jinsi ya Kutuma maombi

Maombi yote yaandikwe kwa :-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji Tunduma,
S. L. P 73,
TUNDUMA.

Aidha, maombi yote yawasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma kwa Mkono au yatumwe kwa barua pepe td@tundumatc.go.tz na si vinginevyo.


Josephat W. Kayombo

**KAIMU MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

